# Kuelewa Maendeleo ya Masomo ya Mtoto Wako

Kuelewa maendeleo ya masomo ya mtoto wako ni muhimu kwa mafanikio yake shuleni. Ukijua jinsi anavyofanya katika masomo yake, unaweza kumsaidia na kumwongoza kwa ufanisi. Kuna njia mbalimbali ambazo shule ya mtoto wako inaweza kutumia kutathmini mafundisho yake, kama vile mitihani na majaribio. Mitihani na majaribio haya hutusaidia kufahamu safari yake ya elimu.

Shule itashiriki maendeleo ya mtoto wako kwa njia nyingi. Huenda ikatuma barua pepe au ujumbe wenye alama au matokeo ya mtihani ya mtoto wako. Huenda pia ikatuma barua au kupiga simu nyumbani. Kila shule hufanya mkutano wa wazazi na mwalimu ambapo familia yako inaweza kukutana na mwalimu ili mjifunze kuhusu maendeleo ya mtoto wenu. Ni muhimu kuhudhuria mikutano hii. Ikiwa huna ujuzi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza, unaweza kuomba huduma ya mkalimani. Zungumza na mwalimu wa mtoto wako ili ujue machaguo yako. Unaweza pia kujifunza kuhusu wakalimani katika sehemu yetu ya kutumia huduma za wakalimani.

Kuelewa maendeleo ya masomo ya mtoto wako hukuwezesha kumsaidia mtoto wako. Ukiona nyanja zinazompa changamoto, unaweza kutoa msaada wa ziada. Baadhi ya machaguo ni pamoja na kutoa mafunzo au mazoezi ya ziada nyumbani. Kusherehekea mafanikio na juhudi yakepia zitawahamasisha kuendelea kufanya kazi kwa bidii. Endelea kusoma ili ujifunze jinsi ya kumsaidia mtoto wako na jinsi shule zinavyoangalia maendeleo ya mtoto wako.

## Je, unaweza kusaidia kuelewa maendeleo ya masomo ya mtoto wako vipi?

**Hata kama una shughuli nyingi**, bado unaweza kumsaidia mtoto wako. Mwulize kuhusu jinsi anavyofanya na mambo anayojifunza shuleni. Wanapokuwa wakubwa, unaweza kumhimiza waombe msaada kutoka kwa shule zao. Wanaweza kujiunga na mipango ili kuwasaidia

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

kujifunza na kukua. Kuna baadhi ya mawazo na mifano zaidi hapa.

Unaweza kumsaidia mtoto wako hata kama Kiingereza si lugha yako ya kwanza au kama uzoefu wako na shule ulikuwa tofauti. Unaweza kumsaidia mtoto wako kwa njia nyingi.

## Fuatilia maendeleo ya mtoto wako.

Unaweza kufanya hivyo kwa njia kadhaa. Shule nyingi hutumia vituo vya mtandaoni ili kuipa familia taarifa iliyosasishwa kuhusu maendeleo ya mtoto wao. Baadhi ya vituo vya kawaida vya mtandaoni ni pamoja na Campus Infinite, Class Dojo, Bloomz, na Power School. Unaweza pia kumwuliza mwalimu wa mtoto wako au wafanyakazi wengine wa shule. Mara nyingi, walimu hushiriki kuhusu maendeleo ya mtoto wako wakati wa hafla za shule kama mikutano ya wazazi na walimu.

## Pata taarifa iliyosasishwa.

Mtoto wako anaweza kusahau kushiriki taarifa au vijitabu vya maelekezo anavyopewa shuleni. Akiwa mdogo, unaweza kuangalia mkoba wake wa kubebwa mgongoni ili uone kazi za shuleni za kufanywa nyumbani au mawasiliano mengine yaliyotumwa na shule.

## Waulize walimu kuhusu jinsi wanavyotuza alama za kazi ya wanafunzi.

Waulize walimu wa mtoto wako kuhusu jinsi wanavyotuza alama za kazi za wanafunzi na jinsi wanavyofuatilia maendeleo yao. Waulize jinsi watakavyoshiriki taarifa hii na wewe. Ni vyema kumwuliza mwalimu mwanzoni mwa mwaka wa masomo au darasa. Ukifanya hivyo, wewe na mtoto wako mtaweza kuzungumza kuhusu maendeleo yake huku akijifunza. Hakuna muda wa mwisho wa kuuliza jinsi mtoto wako anavyopewa alama na kutathminiwa.

### Unaweza kuuliza:

- Je, njia gani ni bora ya kuwasiliana nawe ikiwa nina maswali kuhusu alama au maendeleo ya masomo ya mtoto wangu?
- Je, huwa unatathmini vipi kazi ya mtoto wangu?
- Je, ninaweza kuangalia wapi alama za mtoto wangu?
- Je, ninaweza kujifunza vipi kuhusu maendeleo ya mtoto wangu?

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

### Waulize walimu kuhusu jinsi watakavyoshiriki maendeleo na alama za mtoto wako.

Shule nyingi hutumia programu ya mtandaoni kuandika alama za wanafunzi, alama za mtihani, au matokeo ya tathmini. Shule ina wajibu wa kusaidia familia kupata programu hizi za mtandaoni. Lazima zisaidie familia kuelewa taarifa kuhusu alama za mtoto wao au matokeo mengine. Ikiwa unaona kuwa programu ya mtandaoni haikusaidii au ikiwa haipatikani katika lugha unayopendelea, unaweza kuomba kuona alama au matokeo ya mtoto wako kwa njia tofauti. Unaweza kupata matokeo hayo kupitia barua pepe, ana kwa ana, au kwa simu.

#### Unaweza kuuliza:

- Nina shida ya kutazama alama za mtoto wangu mtandaoni. Je, kuna njia nyingine ya kuona alama zake?
- Je, ninaweza kupata wapi msaada wa kuona alama za mtoto wangu? Vipi kuhusu matokeo ya tathmini yake?
- Je, ninaweza kukutana nawe vipi ili nijue zaidi kuhusu mafundisho na alama za mtoto wangu?

## Je, unaweza kumsaidia mtoto wako kujifunza vipi akiwa na umri tofauti?

### Msaidie mtoto wako akiwa katika shule ya msingi.

Unaweza kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako ili umwulize kuhusu mafundisho ya mtoto wako na jinsi unavyoweza kumsaidia. Unaweza kumwuliza jinsi anavyotuza alama za wanafunzi au tathmini watakazofanya. Ikiwa mtoto wako ni mdogo, unaweza kuzungumza na mwalimu. Mwulize jinsi anavyotuza alama za wanafunzi au tathmini watakazofanya. Pata mawazo kuhusu jinsi unavyoweza kumsaidia mtoto wako kujifunza nyumbani. Unaweza pia kushiriki taarifa kuhusu mtoto wako na jinsi anavyopenda kujifunza. Ikiwa mtoto wako ana tatizo, amechoshwa, au ana wasiwasi kuhusu kazi ya shule, unaweza pia kutaka kushiriki

taarifa hiyo na mwalimu. Kumbuka kuwa unaweza kuzungumza kuhusu alama na maendeleo ya mtoto wako wakati wa mikutano ya wazazi na mwalimu ambapo jambo hili huwa mada ya mazungumzo mara nyingi. Omba huduma za wakalimani mapema, ikiwa zinahitajika.

Huenda ukawa na wasiwasi unapozungumza na mwalimu. Kumbuka kwamba ni muhimu kwa familia, walimu, na shule kuwa na mawasiliano mazuri ili kusaidia mtoto wako.

## Msaidie mtoto wako akiwa katika shule ya kati na upili.

Watoto wanapokuwa wakubwa, wanaweza kusimamia mafundisho yao zaidi. Watoto wa shule za kati na upili huelewa alama vizuri zaidi. Huwa wanaelewa mambo wanayohitaji kufanya shuleni vizuri zaidi kuliko watoto wadogo.

- Zungumza na mtoto wako kuhusu alama na mafundisho yake. Kufanya hivyo kunaonyesha mtoto wako kwamba unaamini uwezo wake wa masomo. Mruhusu awajibike kwa elimu yake.
- Mfundishe mtoto wako kwamba anaweza kuomba msaada wakati anahitaji msaada. Ni muhimu kuzungumza na watoto wako kuhusu shule katika mwaka mzima wa masomo.
- Mtoto wako anapohisi kuwa amechanganyikiwa, amekata tamaa, au anahitaji msaada zaidi, huenda akasaidika akikutana na mwalimu. Wakati mwingine, huenda wazazi au walezi kuhudhuria mkutano huo ukasaidia. Wakati mwingine, mtoto wako anaweza kukutana na mwalimu peke yake. Mtoto wako anaweza tu kuzungumza na mwalimu wake kabla au baada ya darasa. Mtoto wako akikutana na mwalimu peke yake, unaweza kumwuliza mtoto wako kuhusu jinsi mazungumzo yalivyokwenda. Mpongeze kwa kuomba msaada na kuwajibika kwa elimu yake.

### Unaweza kumwuliza mtoto wako:

#### Maswali kuhusu alama

- Je, unahisi vipi kuhusu alama zako?
- Je, huwa unatuzwa alama vipi katika mafunzo yako?

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

- Je, huwa unajuaje alama zako?

### Maswali kuhusu maendeleo ya mtoto wako

- Je, unaendelea vipi shuleni?
- Je, unahisi vipi kuhusu maendeleo yako shuleni?
- Je, huwa unafurahia kujifunza kuhusu masomo au mada gani?
- Je, unaamini kuwa unaelewa masomo gani vizuri zaidi?

### Maswali ya kumsaidia kujifunza

- Je, unafikiri kuwa unaweza kuboresha nyanja gani?
- Je, huwa unahisi wasiwasi kuhusu mafunzo yako yoyote?
- Je, huwa unahitaji kujitahidi sana katika mada au masomo gani?
- Je, ungependa usaidiwe zaidi katika masomo au nyanja gani?
- Je, unahisi kuwa unapata msaada unaohitaji ili ufaulu?
- Je, ninaweza kukusaidia vipi?

## Njia Tofauti Ambazo Shule Hutumia Kuangalia Maendeleo ya Masomo

Matokeo ya tathmini na mtihani huchangia sana katika kuelewa maendeleo ya masomo ya mtoto wako. Matokeo huonyesha nyanja ambazo mtoto wako anafanya vizuri na nyanja anazoweza kuboresha. Kadi za ripoti za mtoto wako, alama za mtihani, na maoni ya mwalimu pia ni njia za kuangalia maendeleo yake. Unaweza kujifunza zaidi katika sehemu hii.

### Tathmini na Mitihani ya Jimbo

Tathmini hutumiwa kujifunza kuhusu maendeleo ya masomo ya wanafunzi. Zinajumuisha mitihani ya kawaida, na pia shughuli za darasani. Shughuli hizi husaidia waalimu kubainisha wakati ambapo kila mwanafunzi anahitaji msaada au mazoezi ya ziada na wanapokuwa tayari kusonga mbele.

> Tathmini pia hutumiwa kuangalia ujuzi wa Kiingereza wa wanafunzi. Wanafunzi walio na viwango vya chini vya usatdi wa lugha ya Kiingereza huchukuliwa kuwa Wanafunzi

wa Kiingereza. Huwa wanafanya mtihani wa Kiingereza kila mwaka ili kuangalia maendeleo yao.

Mitihani ya jimbo hupima maendeleo ya masomo ya wanafunzi kulingana na Viwango vya Kujifunza vya Ohio katika nyanja fulani za masomo. Matokeo ya mtihani pia husaidia kupima utendaji wa kila shule ya umma ambayo huwekwa wazi kwenye Kadi ya Repot ya Shule ya Ohio.

Wanafunzi wa darasa la tatu hadi darasa la nane na shule ya upili hufanya mitihani ya Jimbo la Ohio katika sanaa ya lugha ya Kiingereza na hisabati. Katika shule ya kati na ya upili, wanafunzi wanaweza kufanya mitihani ya sayansi na masomo ya kijamii.

Taarifa zaidi kuhusu Mitihani ya Jimbo la Ohio inapatikana kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

**Alama hutumiwa kupima kazi za shule za wanafunzi.** Kila shule inaweza kutuza wanafunzi alama kwa njia tofauti. Walimu katika shule hiyo pia wanaweza kutuza alama kwa njia tofauti. Baadhi ya mifumo ya kutuza alama hujumuisha tu tathmini za darasa au mitihani lakini haijumuishi kazi za shuleni za kufanywa nyumbani. Mifumo mingine huzingatia umahiri wa mafundisho. Kuna hata kadi za ripoti zinazozingatia viwango. Kuna mifumo mingi kiasi kwamba hatuwezi kuorodhesha yote hapa. Lakini familia zinahitaji kuelewa mfumo ya shule na mwalimu wao ya kutuza alama. Ni muhimu kuuliza shule yako na walimu wa mtoto wako ili ujue jinsi wanavyotuza alama. Kuna baadhi ya njia za kawaida ambazo wanafunzi hutuzwa alama huko Ohio hapa.

## Kutuza Alama katika Shule ya Msingi na Elimu ya Utotoni

Katika miaka ya kwanza ya shule, kama vile katika shule ya chekechea na shule ya msingi, shule inaweza kutumia herufi ili ziwakilishe alama za wanafunzi. Kila herufi inawakilisha neno linaloelezea jinsi mtoto amejifunza ujuzi au dhana.

**Mifano ya vielezo vya kawaida vya kutuza alama:**

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

| Herufi | Maana |
|---|---|
| O | Outstanding (Vizuri Kabisa) |
| S | Satisfactory (Vizuri Kiasi) |
| N | Needs improvement (Anahitaji Kuboresha Ujuzi) |
| U | Unsatisfactory (Alama Duni) |

| Herufi | Maana |
|---|---|
| E | Exceeds expectations (Vizuri kuliko matarajio) |
| M | Meets expectations (Ametimiza matarajio) |
| P | Progressing (Anaendelea vizuri) |
| I | Insufficient progress (Haendelei vizuri) |

## Kutuza Alama katika Shule ya Kati na Shule ya Upili

Shule za upili na za kati pia zinaweza kutumia herufu ili ziwakilishe alama. Herufi huwakilisha tarakimu ambayo kwa kawaida huwa kati ya sifuri na 100. Tarakimu ndogo huwakilisha alama ya chini. Tarakimu kubwa huwakilisha alama bora (ya juu).

Alama za wanafunzi zinaweza kutolewa kutoka kwa jumla ya 100. Hii inategemea jinsi wanavyofanya vizuri katika tathmini au kazi. Baadhi ya shule zinaweza kutoa alama 10 (kielezo cha kutuza alama cha pointi 10). Shule nyingine zinaweza kutoa alama saba (kielezo cha kutuza alama cha pointi 7).

Hii ina maanishwa kwamba katika kielezo cha kutuza alama cha pointi 10, tofauti kati ya alama moja na nyingine ni pointi 10. Katika kielezo cha kutuza alama cha pointi 7 tofauti ni pointi saba.

Kwa njia yoyote, vielezo vyote vya kutuza alama hutumia herufi ya A kuwakilisha alama ya juu na herufi ya F kuwakilisha alama ya chini kabisa.

**Mifano ya vielezo vya kutuza alama ni:**

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

| Herufi | Kielezo cha kutuza alama cha pointi 10 | Kielezo cha kutuza alama cha pointi 7 |
|---|---|---|
| A | 100 – 90 | 100 – 93 |
| B | 89– 80 | 92 – 85 |
| C | 79 – 70 | 84 – 78 |
| D | 69 – 60 | 77 – 70 |
| F | 59 na chini | 69 na chini |

### Wastani wa Pointi ya Alama (Grade Point Average (GPA)

Katika shule ya kati na ya upili, alama za wanafunzi zinaweza jumlishwa na kuandikwa katika Wastani wa Pointi ya Alama (au GPA). GPA ya mwanafunzi ni alama ambayo waajiri, vyuo, au vyuo vikuu vinaweza kukagua kwa ajili ya ufadhili wa masomo au fursa za kazi.

## Kadi za Ripoti

Shule hutumia kadi za ripoti kushiriki alama za mwisho na familia na wanafunzi. Zinaweza kutumwa nyumbani au kuchapishwa mtandaoni. Kadi za ripoti ni sehemu ya kumbukumbu ya kudumu ya mwanafunzi katika shule.

## Ripoti za Maendeleo

Shule nyingi hutumia familia ripoti ya maendeleo baada ya miezi michache ya mwaka wa masomo. Ripoti hii husaidia familia na wanafunzi kujua jinsi mtoto wao anavyojifunza mafunzo yanayofundishwa shuleni. Ripoti hii inaweza kusaidia walimu na familia kuelewa nyanja ambazo mwanafunzi anapata alama nzuri kabisa na nyanja anazoweza kuboresha.

Uliza shule yako ili ujue wakati na jinsi familia zinavyopewa kadi za ripoti au ripoti za maendeleo.

## Rasilimali za Ziada

Unaweza kupata rasilimali na taarifa zaidi kuhusu kutuza alama hapo chini.

- Unaweza kujifunza zaidi kutoka kwa sehemu ya "Kumsaidia Mtoto Wako Kufaulu Shuleni" ya Zana ya Familia ya NCELA ukichagua Sura ya 6. Inapatikana katika lugha

nne (Kiiingereza, Kiarabu, Kichina, na Kihispania). https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit

- Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako kwenye tovuti ya Colorin Colorado. https://www.colorincolorado.org/article/talk-your-childs-teacher
- Rasilimali ya Soma Kadi ya Ripoti (Read a Report Card) katika nyenzo ya Reading Rockets hutoa taarifa zaidi. https://www.readingrockets.org/article/how-read-report-card
- Jifunze kuhusu njia ishirini unazoweza kutumia kumsaidia mtoto wako kwenye tovuti ya Colorin Colorado. https://www.colorincolorado.org/article/twenty-ways-you-can-help-your-children-succeed-school
- Ukurasa wa USA Hello kuhusu jinsi ya kumsaidia mtoto wako shuleni unapatikana katika lugha nyingi. https://usahello.org/education/children/help-child-in-school
- Rasilimali ya Kuangalia Mafanikio ya Mtoto Wangu kwa Makini (Taking a Closer Look at My Child's Academic Success) kutoka kwa nyenzo ya Reading Rockets huelezea jinsi familia zinavyoweza kusaidia mtoto wao kufaulu katika masomo. https://www.readingrockets.org/article/taking-closer-look-my-childs-academic-success
- Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu kuwasaidia watoto katika shule ya kati kwenye tovuti ya Kituo cha Ushiriki wa Familia cha Jimbo Nzima la Ohio (Ohio Statewide Family Engagement Center). https://ohiofamiliesengage.osu.edu/resources/launching-your-middle- schooler-to-success-available-in-chinese-somali-nepali-spanish-and-arabic
- Maktaba yako ya umma inaweza kuwa rasilimali nzuri ya kumsaidia mtoto wako kupata alama nzuri. Mbali na upatikanaji wa vitabu bure, maktaba nyingi za umma hutoa msaada wa kazi shuleni za kufanywa nyumbani na mafunzo bure. Zinaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza mtandaoni. Zinaweza pia kuwasaidia kufikia kompyuta, intaneti, na teknolojia nyingine ambazo wanaweza kuhitaji. Ili uapte

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

maktaba ya umma iliyo karibu nawe tembelea tovuti ya Library Ohio. https://library.ohio.gov/using-the-library/find-an-ohio-library

- Tovuti ya bure ya Kuandika na Kuimarisha Ujuzi (Write and Improve) husaidia wanafunzi kuboresha uandishi wao. https://writeandimprove.com/free

*Rasilimali hizi zinalenga kuimarisha masomo, ustawi wa wanafunzi, na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa Ohio wanaozungumza lugha nyingi. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi za kushirikiana kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) na Kituo cha Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio cha Elimu na Mafunzo ya Kazi (The Ohio State University's Center on Education and Training for Employment) pamoja na kikundi cha kujitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University